TANGAZO LA SERIKALI NA. 93 la tarehe 17/2/2023

SHERIA YA MISITU,
(SURA 323)

# NOTISI

(*Imetengenezwa chini ya vifungu vya 23 na 29(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUREKEBISHA MPAKA WA ENEO LA MSITU WA HIFADHI YA MIKOKO KILWA MASOKO, 2023

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kurekebisha Mpaka wa Eneo la Msitu wa Hifadhi ya Mikoko Kilwa Masoko, 2023.

Eneo linalopendekezwa kuchukuliwa

2. Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Mikoko Kilwa Masoko lenye ukubwa wa hekta 1.644 sawa kilometa za mraba 0.02 lililoainishwa katika Jedwali la Notisi hii linapendekezwa kurekebishwa na kuondolewa kutoka katika Msitu wa Hifadhi ya Mikoko Kilwa Masoko kuwa eneo la ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko.

Matumizi ya eneo

3. Madhumuni ya kupendekeza kurekebisha mpaka wa eneo la Msitu wa Hifadhi ya Mikoko Kilwa Masoko ni-

(a) kutenga eneo lenye ukubwa wa hekta 1.644 sawa na kilometa za mraba 0.02 kutoka katika Msitu wa Hifadhi ya Mikoko Kilwa Masoko kwa ajili ya kufanikisha mradi wa Serikali Kuu wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko; na
(b) kuendelea kuhifadhi, kuendeleza, kusimamia na kutumia kwa uangalifu rasilimali za misitu ndani ya eneo la Hifadhi ya Msitu wa Mikoko Kilwa Masoko litakalobaki baada ya kurekebisha mpaka ili

kuongeza mchango wa sekta ya misitu katika maendeleo endelevu ya Tanzania.

Muda wa notisi

4. Notisi hii itakuwa halali kwa siku tisini (90) kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, na ndani ya kipindi hicho, mtu au kikundi cha watu au mwakilishi wao wanaweza, kwa maandishi-

(a) kupinga;
(b) kuwasilisha maoni; au
(c) kudai haki zozote zilizopo katika eneo husika zinazotokana na sheria za kimila au mazao ya msitu au haki zozote zinatokana na sheria nyingine katika eneo linalopendekezwa kuondolewa kutoka Msitu wa Hifadhi ya Mikoko Kilwa.

Mipaka ya Msitu wa Hifadhi

5. Mpaka wa Msitu wa Hifadhi ya Mikoko Kilwa Masoko utaendelea kuwa Bahari ya Hindi kwa upande wa Magharibi na bamvua la juu la Bahari ya Hindi kwa upande wa Kaskazini, Mashariki na Kusini mwa Hifadhi hiyo ya Mikoko ya Kilwa Masoko.

Uwasilishwaji wa mapingamizi

6. Mapingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya Notisi ya kusudio la kurekebisha mpaka wa msitu wa Hifadhi wa Mikoko Kilwa Masoko ili kuondoa eneo lenye ukubwa wa hekta 1.644 sawa na kilometa za maraba 0.02 kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko yanaweza kuwasilishwa kwa Waziri kupitia anuwani ifutayo-

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA

*Tangazo la serikali na. 93 (linaendelea)*

---

JEDWALI

---


*(Limetengenezwa chini ya aya 2)*

WILAYA YA KILWA

MPAKA WA MSITU WA MIKOKO KILWA MASOKO UNAOKUSUDIWA KUREKEBISHWA ILI KUONDOA ENEO LENYE UKUBWA WA HEKTA 1.644 SAWA NA KILOMETA ZA MRABA 0.02 KWA AJILI YA UJENZI WA BANDARI YA UVUVI KILWA MASOKO

*Makadirio ya eneo:* Hekta 1.644 sana na  Kilometa za Mraba 0.002 Eneo lilipo na Mipaka

Sehemu ya eneo la Msitu wa Hifadhi ya Mikoko Kilwa linalopatikana katika Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi kama lilivyobainishwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 3155 ya Septemba, 2022 (Skeli 1:1000) lenye ukubwa wa takribani hekta 1.644  sawa na  Kilometa za Mraba 0.02 iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dodoma  na yenye mipaka ifuatayo:




Dodoma,
30 December, 2022

PINDI H. CHANA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*